

# Wakati Mfanyakazi wa Kijamii kutokaldara ya Huduma kwa Familia Anakutembelea Nyumbani Mwako



## Una haki ya:

- Kuitisha *Kitambulisho cha Mfanyakazi wa Jimbo* kabla ya kumkaribisha mfanyakazi huyo nyumani mwako;
- Kupiga simu kwa ofisi inayofaa ya Idara ya Huduma za Familia kuthibitisha utambulisho wa mfanyakazi huyo;
- Kuuliza maswali ikiwa unataka kuelewa kile mfanyakazi huyo anafanya au kukuambia ufanye;
- Kukataa na kisha kuuliza kuongea na msimamizi wa mfanyakazi huyo ikiwa haufurahishwi na maswali unayoulizwa;
- Kuuliza kuona amri ya mahakama ikiwa mfanyakazi huyo anataka kuondoa mtoto wako kutoka nyumbani mwako; na
- Kupiga simu kwa 911 au polisi wa karibu ikiwa unashuku mtu huyo anajisingizia kuwa mfanyakazi wa kijamii wa FSD.

## Unaweza kutarajia yafuatayo:

- Ikiwa mfanyakazi anahitajika kuzunguka na kukagua nyumba yako, lazima aombe ruhusa yako. Ikiwa haufurahishwi na jambo hili, mfanyakazi huyo atakuzungumzia kuhusu hatua zifuatazo zinazoweza.
- Mfanyakazi huyo anaweza kukuuliza maswali kuhusu wanafamilia wote, marafiki, na watu wengine wanaoweza kukusaidia.
- Mfanyakazi huyo anaweza kuuliza nguo ya mtoto iinuliwe au itolewe aone mchubuko au jeraha la kimwili kwenye mtoto. Hii itafanywa mbele ya mtu mwingine mzima. Mfanyakazi huyo anaweza kukuambia umpeleke mtoto kwa daktari.
- Mfanyakazi huyo anaweza kutaka kuzungumza na moto kando kuhusu vile mambo yanaendelea. *Sio lazima* mfanyakazi huyo awe peke yake na mtoto. Wanaweza, kwa mfano, kuketi kwenye ukumbi au mahali pengine unapoweza kumuona moto wako bila kusikia mazungumzo yao.

### Ofisi za Wilaya za Huduma kwa Familia

**Barre:** (802) 479-4260

**Bennington:** (802) 442-8138

**Brattleboro:** (802) 257-2888

**Burlington:** (802) 863-7370

**Hartford:** (802) 295-8840

**Middlebury:** (802) 388-4660

**Morrisville:** (802) 888-4576

**Newport:** (802) 334-6723

**Rutland:** (802) 786-5817

**Springfield:** (802) 885-8900

**St. Albans:** (802) 527-7741

**St. Johnsbury:** (802) 748-8374

*Baada ya masaa, wikendi, au sikukuu za jimbo, piga simu  
kwa 1-800-649-5285.*

<http://dcf.vt.gov/fsd>